# CHUO CHA AFYA BLUE PHARMA

## Fomu ya Maelekezo ya Kujiunga na Chuo

## Mwaka wa Masomo: 2025/2026




**Chuo cha Afya Blue Pharma**
**S.L.P 1570,**
**Manispaa ya Singida,**
**www.bphacoh.ac.tz**
**info@bphacoh.ac.tz**
**0743358048**

**bluepharmacollegeofhealth**

## UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Afya Blue Pharma kwa ajili ya mafunzo ya kozi ya Famasi katika ngazi ya Stashahada. Unatakiwa kuwasili chuoni mnamo **tarehe 21 September 2025** kwa ajili ya usajili na kuhudhuria programu ya ukaribisho (Orientation) na kufundishwa kozi ya awali (Pre – Course) ya Hisabati na Kingereza yanayotarajia kuanza **tarehe 28 Septemba 2025** ambayo itakuwezesha kusoma vema kozi ya Famasi. Unakumbushwa kuwa mwanafunzi hataruhusiwa kuendelea na masomo chuoni ikiwa kama hajahudhuria kikamilifu programu ya ukaribisho (Orientation Program) na kozi ya awali ya Hisabati na Kingereza.

## MAELEKEZO YA KUFIKA CHUONI

Chuo kinapatikana Singida Mjini katika Ghorofa la Blue Plaza karibu na jengo la TRA. Kwa mwanafunzi atakayetokea Mkoani na kushushwa katika Stendi kubwa ya Misuna, au anatokea ndani ya Mkoa wa Singida na kushushwa katika Stendi ya Msufini, atatakiwa kuchukua usafiri wa Bajaji au Pikipiki na kupelekwa katika Ghorofa la Blue Plaza. Gharama kwa bajaji ni shilingi za kitanzania 500/= na kwa Pikipiki ni shilingi za kitanzania 1,000/=.

## NYARAKA ANAZOTAKIWA KUWASILI NAZO WAKATI WA USAJILI

Mwanafuzi atawasili katika ofisi ya usajili akiwa na vitu vifuatavyo

i. Barua ya usajili (Admission Letter) uliyotumiwa na Chuo pamoja na fomu hii ambayo imejazwa kikamilifu katika kiambatanisho Na. 1 & 2

ii. Picha moja (1) ya passpoti size ya rangi ikiwa imeandikwa nyuma jina kamili la mhusika (mwanafunzi).

iii. Cheti halisi cha taaluma kidato cha Nne na nakala yake iliyothibitishwa na Mwanasheria (certified copy).

iv. Cheti halisi cha kuzaliwa na nakala yake iliyothibitishwa na Mwanasheria (certified copy) au uthibitsho wa mahakama (affidavit).

v. Nakala halisi ya malipo kutoka bank (bank pay in slip) kwa ada na michango mingine.

vi. Fomu ya matibabu (medical examination form) iliyojazwa kikamilifu (ipo kwenye tovuti ya Chuo *www.bphacoh.ac.tz*).

vii. Nakala ya kitambulisho cha Bima ya Afya kwa Mwanafunzi aliyekwishajiunga na Bima

ya afya.

viii. Kitambulisho na hati ya kusafiria (Travelling Passport) kwa ambao siyo raia wa Tanzania.

ix. Barua ya ruhusa kwa mtumishi ambaye anasoma wakati akiwa bado yuko kazini.

**TAHADHARI:** Ni kosa la jinai kisheria kuleta/ kuwasilisha taarifa za uongo. Hatua kali zitachukuliwa kwa atakae jaribu au kufanya kosa hilo.

**MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE**

i. Mwanafunzi atatakiwa kulipa ada na michango mingine ili aweze kusajiliwa na kuendelea na masomo chuoni. Ada italipwa walau kwa awamu Tano (5) na michango mingine yote italipwa kwa awamu mbili (2), wakati wa kuwasili chuoni.

ii. Awamu ya kwanza ya malipo ya ada itafanyika mwanzoni mwa muhula wa kwanza wa mwaka wa masomo, awamu ya pili italipwa katikati ya muhula wa kwanza, awamu ya tatu italipwa mwishoni mwa muhula wa kwanza, awamu ya nne italipwa mwanzoni mwa muhula wa pili na awamu ya tano italipwa katikati ya muhula wa pili wa mwaka wa masomo. (Tarehe za mwisho wa malipo ya kila awamu zinapatikana katika fomu ya maelekezo ya ulipaji wa ada na michango mingine inayopatikana kwenye tovuti ya chuo: *www.bphacoh.ac.tz )*

Majedwali hapo chini yanabainisha ada na michango mingine itakayotakiwa kulipwa na Mwanafunzi:

a. Ada ya mafunzo

| | |
|---|---|
| Basic Technician Certificate in Pharmaceutical science (**NTA Level 4**) | Tshs 1,600,000/= |
| Technician Certificate in pharmaceutical science (**NTA Level 5**) | Tshs 1,600,000/= |
| Ordinary Diploma in Pharmaceutical Science (**NTA Level 6**) | Tshs 1,600,000/= |

b. Michango mingine kwa Mwaka wa kwanza na wanafunzi wapya

| Na. | Maelezo | Kiasi (Tshs) | | Ulipaji |
|---|---|---|---|---|
| | | Kutwa | Bweni | |
| 1 | Ada ya usajili wa kila Mwaka | 10,000.00 | 10,000.00 | Kila Mwaka |
| 2 | Ada ya mitihani ya mwisho wa muhula wa kwanza | 150,000.00 | 150,000.00 | Kila Mwaka |
| 3 | Bima ya afya | 60,000.00 | 60,000.00 | Kila Mwaka |
| 4 | Mafunzo kwa vitendo | 150,000.00 | 150,000.00 | Kila Mwaka |
| 5 | Pesa ya dharula | 50,000.00 | 50,000.00 | Mara Moja |
| 6 | Serikali ya wanafunzi | 10,000.00 | 10,000.00 | Kila Mwaka |
| 7 | Pesa ya udahili | 50,000.00 | 50,000.00 | Mara Moja |
| 8 | Ada ya mitihani ya mwisho wa muhula wa pili | 150,000.00 | 150,000.00 | Kila Mwaka |
| 9 | Kitambulisho cha Mwanafunzi | 10,000.00 | 10,000.00 | Mara Moja |
| 10 | Koti jeupe la Maabara | 30,000.00 | 30,000.00 | Mara Moja |
| 11 | Mahafari | 50,000.00 | 50,000.00 | Mara Moja |
| 12 | Majaribio endelevu | 50,000.00 | 50,000.00 | Kila Mwaka |
| 13 | Sare ya Chuo | 100,000.00 | 100,000.00 | Mara Moja |
| 14 | Pesa ya NACTVET kudhibiti na kuhakikisha Ubora | 25,000.00 | 25,000.00 | Kila Mwaka |
| 15 | Bweni | - | 400,000.00 | Kila Mwaka |
| | Jumla | 895,000.00 | 1,295,000.00 | |

c. Michango mingine kwa mwaka wa pili (NTA level 5) na wa tatu (NTA level 6)

| Na. | Maelezo | Kiasi (Tshs) | |
|---|---|---|---|
| | | Kutwa | Bweni |
| 1 | Ada ya usajili wa kila Mwaka | 10,000 | 10,000 |
| 2 | Ada ya mitihani ya mwisho wa muhula wa kwanza | 150,000 | 150,000 |
| 3 | Bima ya afya | 60,000 | 60,000 |
| 4 | Mafunzo kwa vitendo | 150,000 | 150,000 |
| 5 | Pesa ya dharula | - | - |
| 6 | Serikali ya wanafunzi | 10,000 | 10,000 |
| 7 | Pesa ya udahili | - | - |
| 8 | Ada ya mitihani ya mwisho wa muhula wa pili | 150,000 | 150,000 |
| 9 | Kitambulisho cha Mwanafunzi | - | - |
| 10 | Koti jeupe la Maabara | - | - |
| 11 | Mahafari | - | - |
| 12 | Majaribio endelevu | 50,000 | 50,000 |
| 13 | Sare ya Chuo | - | - |
| 14 | Pesa ya NACTVET kudhibiti na kuhakikisha Ubora | 25,000 | 25,000 |
| 15 | Bweni | - | 400,000 |
| **Jumla** | | **605,000/=** | **1,005,000/=** |

iii. Malipo ya bweni yatafanyika kwa awamu mbili; Mwanzoni mwa muhula wa kwanza na mwanzoni mwa muhula wa pili wa masomo.

iv. Malipo kwa njia ya mitandao ya simu kama vile; MPesa, Mixx by Yas, Airtel Money na mitandao mingine kama hiyo **HAYATARUHUSIWA**.

v. Malipo ya ada na michango mingine itatakiwa kulipwa katika nambari zilizo orodheshwa kwenye jedwali hapo chini pasipo kuzichanganya:

| JINA LA BENKI | JINA LA AKAUNTI | NAMBARI YA AKAUNTI | MALIPO KWA AJILI YA |
|---|---|---|---|
| CRDB | BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH | 0150417961300 | ADA |
| CRDB | BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH | 0150417961301 | MICHANGO MINGINE |

vi. Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kutumia pesa ya ada na michango mingine kwa matumizi mengine binafsi, hivyo inashauriwa pesa kulipwa moja kwa moja kwenye akaunti zilizoorodheshwa kwenye jedwali hapo juu.

vii. Mabadiliko yoyote ya ada au/na michango mingine yatawasilishwa kwa Mfadhili wa mwanafunzi kwa maandishi na Mkuu wa Chuo. Chuo hakitahusika na udanganyifu wowote kuhusiana na mabadiliko ya gharama za mafunzo yatakayowasilishwa kwa Mfadhili na mwanafunzi husika pasipo barua ya Mkuu wa Chuo.

**CHAKULA NA MALAZI**

i. Chuo kinatoa Malazi kwa wanafunzi wa kike na kiume wenye uhitaji. Mwanafunzi atapatiwa malazi baada ya kulipa gharama husika kama zilivyobainishwa kwenye jedwali la michango mingine.

ii. Mwanafunzi atakayekaa bweni la Chuo atakuta vifaa kama vile: Kitanda, Godoro na huduma ya maji na umeme.

iii. Chakula kinapatikana katika mgahawa wa chuo kwa bei himilifu. Hatahivyo, ikiwa Mwanafunzi atahitaji kupatiwa chakula na Chuo, anatakiwa kulipa kiasi cha shilingi milioni moja na nusu (1,500,000/=) kwa mwaka wa masomo.

**Muhimu**: Mzazi/Mfadhili/Mlezi unashauriwa yafuatayo kwa ajili ya maendeleo ya mwanafunzi awapo chuoni:

a. Mwanafunzi anashauriwa kuishi katika mabweni ya Chuo kwa ajili ya uangalizi wa karibu hasa nyakati zisizo za masomo ya darasani.

b. Mwanafunzi apewe pesa ya matumizi kwa ajili ya chakula (milo mitatu) na mahitaji mengine ya kijamii.

## AFYA NA GHARAMA ZA MATIBABU

i. Mwanafunzi anapaswa kupima afya yake na kujaza fomu ya uthibitisho wa afya iliyoambatanishwa na fomu hii. Ni muhimu kwa uongozi wa Chuo kufahamu hali ya kiafya ya mwanafunzi hasa kama ana ugonjwa wa kudumu ili kuweza kumuwekea mazingira wezeshi na rafiki kutokana na hali yake muda wote awapo chuoni.

ii. Mwanafunzi atatakiwa kuwa na Bima ya Afya kwa ajili ya kuwa na uhakika wa kupata matibabu kwa kipindi chote awapo mafunzoni. Kwa mwanafunzi ambaye hatakuwa na bima ya afya binafsi, atatakiwa kulipia kiasi kilichobainishwa kwenye jedwali la michango mingine hapo juu kwa ajili ya kukatiwa Bima ya Afya.

iii. Mzazi/Mfadhili/Mlezi wa mwanafunzi atawajibika kuongeza pesa za matibabu ya mwanafunzi ikiwa kama bima ya afya haitojitosheleza kutokana na ukubwa wa tatizo la kiafya.

iv. Uongozi wa chuo hautamuendekeza mwanafunzi ambaye atakuwa na ugonjwa wa kudumu ambao haukuorodheshwa kwenye fomu ya uthibitisho wa afya ya mwanafunzi. Isipokuwa tu kama ugonjwa huo atakuwa ameupata wakati akiwa masomoni.

## GHARAMA ZA KUSAFIRI

Mfadhili wa mwanafunzi ndiye atakayehusika na gharama za mwanafunzi kusafiri kuja au kutoka chuoni.

## SERIKALI YA WANAFUNZI

Chuo kina Serikali ya wanafunzi ambayo inaundwa na viongozi ambao huchaguliwa na wanafunzi kila mwaka. Jukumu la serikali ya wanafunzi huwa ni kusimamia ustawi wa wanafunzi wa Chuo. Kila Mwanafunzi aliyesajiliwa na Chuo anapaswa kuwa Mwanachama wa serikali ya wanafunzi, na anapaswa kulipia kiasi kama ilivyoainishwa katika jedwali la michango mingine hapo juu kila mwaka wa masomo kwa ajili ya kuwezesha serikali kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## KITAMBULISHO CHA MWANAFUNZI

i. Kila mwanafunzi atatengenezewa kitambulisho cha chuo baada ya kuwasilisha picha na kulipia kiasi cha shilingi za kitanzania elfu kumi (10,000/=). Kitambulisho hichi kitapaswa kuvaliwa shingoni na mwanafunzi wakati wowote awapo mafunzoni kwa ajili ya utambulisho.

ii. Endapo itatokea kuwa mwanafunzi amepoteza kitambulisho cha chuo, atatakiwa kulipia kiasi cha shilingi elfu ishirini (20,000/=) na kuwasilisha fomu ya upotevu (loss report) katika ofisi ya muadili wa wanafunzi kwa ajili ya kutengenezewa kitambulisho kingine.

**PESA YA DHARULA (CAUTION MONEY)**

i. Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza au mwanafunzi mpya anaejiunga na Chuo atahitajika kulipa kiasi cha pesa ya dharula kama ilivyoainishwa katika jedwali la michango mingine hapo juu. Pesa hii haitarudishwa kwa mwanafunzi atakapomaliza mafunzo yake.

ii. Pesa hii hazitatumika kufidia uharibifu wa makusudi ambao utafanywa na mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na uvunjaji wa vifaa vya maabara wakati wa mafunzo kwa vitendo.

**SARE**

i. Sare zote (Shati, suruali na koti jeupe kwa wavulana na magauni meupe na koti kwa Wasichana) zitapatika chuoni baada ya mwanafunzi kulipa kiasi kilichobainishwa kwenye jedwali la michango mingine hapo juu.

ii. Kila mwanafunzi atashonewa jozi ya sare zenye ubora ambao unakubalika na uongozi wa Chuo.

iii. Gharama za sare zilizoainishwa kwenye jedwali hazihusishi viatu na soksi, hivyo kila mwanafunzi wa kiume anapaswa kuwasili na jozi ya viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi na jozi walau mbili za soksi nyeupe na ndefu zinazofika kwenye ugoko wa mguu. Mwanafunzi wa kike atatakiwa kuwasili na jozi ya viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi visivyo na kisigino kirefu na walau jozi mbili za soksi nyeupe ndefu zinazofika kwenye sehemu ya ugoko wa mguu.

## VITU VYA KUJANAVYO CHUONI WAKATI WA KUWASILI

Mwanafunzi anapaswa kuwasilisha vitu vifuatavyo kwa ajili ya kusaidia wakati wa kujifunza**:**

i. Kitabu kiitwacho Tanzania Pharmaceutical Handbook (TPH) ambacho kitatumika kama rejea wakati wa mafunzo ya nadharia na vitendo (utengenezaji wa dawa). Kitabu hiki kinapatikana Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa gharama za shilingi za kitanzania elfu hamsini (50,000/=) hivyo Mfadhili wa mwanafunzi anaweza kukinunua moja kwa moja kutoka huko au kulipa kiasi husika chuoni kwa ajili ya manunuzi ya kitabu hicho.

ii. Scientific Calculator (na siyo kikokotozi cha kawaida) kwa ajili ya kujifunza vema katika masomo ambayo yatahusisha hesabu.

iii. Rimu mbili (2) (moja kwa kila muhula) kwa ajili ya kutumika wakati wa kuchapisha mitihani na majaribio ambayo mwanafunzi atayafanya wakati wa mafunzo.

iv. Madaftari (Counter books) 10 za walau 2 quires kwa ajili ya kuandikia vile atakavyokuwa akifundishwa.

v. Kalamu ya wino, kalamu ya risasi, rula na vifaa vinginevyo kadri vitakavyohitajika kwa ajili ya mafunzo.

vi. Kompyuta mpakato (laptop), simu janja, kishikwambi (tablet) au kifaa kingine chochote cha kielekroniki ambacho mwanafunzi anaweza kutunza notisi katika mfumo wa nakala laini (soft copy) kwa ajili ya kujisomea.

vii. Mwamvuli au koti la mvua ambalo litamsaidia mwanafunzi kufika kwa wakati chuoni nyakati za mvua.

## MAHITAJI KWA MWANAFUNZI WA BWENI

Mwanafunzi atakayeishi bweni atahitaji vitu vifuatavyo kwa ajili ya ustawi wake:

i. Walau blanketi moja zito ambalo atalitumia hasa katika misimu ya baridi.

ii. Walau shuka 4

iii. Walau mto mmoja wa kitandani.

iv. Walau Neti moja ya kujikinga na Mbu.

v. Walau Ndoo mbili (2) za plastiki; moja kwa ajili ya kuhifadia maji na nyingine kwa ajili ya kuogea na usafi.

vi. Walau taulo 1

vii. Walau jozi moja ya Kandambili kwa ajili ya kuogea na viatu vya wazi kama vile sandals.

**MAWASILIANO**

i. Taarifa zote muhimu kama maafa au Msiba kutoka nyumbani zitatakiwa kupitia kwa Mkuu wa Chuo na si kwa mwanafunzi moja kwa moja. Ofisi ya Mkuu wa Chuo ndiyo itakuwa na jukumu la kumfikishia mwanafunzi taarifa husika.

ii. Uongozi wa Chuo hautashughulikia changamoto zitakazotokana na mwanafunzi kupewa taarifa kama vile za maafa au Msiba moja kwa moja pasipo kupitia ofisi ya Mkuu wa Chuo.

iii. Barua zote za mwanafunzi kuitwa au kualikwa kwenye vikao au tafrija yoyote zitatakiwa kupitia kwa Mkuu wa Chuo.

iv. Chuo kitawasiliana na mwanafunzi kwa kutoa matangazo kupitia mbao za matangazo za chuo, tovuti ya chuo: *www.bphacoh.ac.tz* , kutumiwa meseji (bulk message) yenye jina la “BLUEPHARMA” au kuandikiwa barua na Mkuu wa Chuo.

**MAFUNZO KWA VITENDO**

Ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira, Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya vitendo katika muhula wa pili wa kila mwaka wa masomo baada ya kuwa amelipa gharama za mafunzo kwa vitendo zilizoainishwa kwenye jedwali la michango mingine.

**MITIHANI NA UTOAJI WA MATOKEO YA MITIHANI**

i. Mwanafunzi atakuwa akifanya majaribio yasiyopungua mawili katika kila muhula wa mwaka wa masomo na mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza na wa pili.

ii. Matokeo ya majaribio na mitihani ya mwisho wa muhula yatatolewa kupitia akaunti ya mfumo wa chuo (SRMIS) ya kila Mwanafunzi.

iii. Kwa kuzingatia kuwa matokeo ni moja ya nyaraka za siri, matokeo yatatolewa kwa namba za usajili za wanafunzi ili kusudi mwanafunzi tu ndiye aweze kuyatambua matokeo yake. Aidha ikiwa Mzazi/Mlezi/Mfadhili atahitaji kuyapata matokeo hayo atapaswa kumuomba mwanafunzi husika ambaye atafuata utaratibu wa kupatiwa matokeo yaliyosainiwa na kugongwa muhuri na Mkuu wa Chuo.

iv. Uongozi wa Chuo unasisitiza kuwa ni vema Mzazi/Mlezi/Mfadhili wa mwanafunzi kufuatilia matokeo ya majaribio na mitihani ya mwisho wa muhula ambayo mwanafunzi atakuwa akifanya wakati wa mafunzo.

**SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO**

i. Chuo kina sheria na taratibu ambazo zitatakiwa kufuatwa kikamilifu na mwanafunzi wakati wote awapo mafunzoni. Sheria na taratibu hizi zitasomwa katika program ya ukaribisho na kuwekwa katika mahali ambapo mwanafunzi atakuwa akizifikia kiurahisi na kuzisoma.

ii. Ni jukumu la kila mwanafunzi kuzisoma, kuzielewa na kuzifuata sheria na taratibu za Chuo.

iii. Zifuatazo ni sheria na taratibu za chuo:

   a. Taratibu za mitihani za mwaka 2022 (Guidelines for assessing CBET Curricula for NTA Programs offered by Health and Allied Sciences Institutions)

   b. Sheria za wanafunzi (Students' Bylaws)

   c. Taratibu za uvaaji wa mavazi (Codes of proper dressing)

**MENGINEYO**

i. Mwanafunzi anategemewa kuwa na tabia njema na kuzingatia maadili ya kitanzania wakati wote wa mafunzo.

ii. Mwanafunzi anategemewa kuwa na hari ya kujituma na kiu ya kujifunza yale ambayo atakuwa akifundishwa darasani.

iii. Mwanafunzi atatakiwa kushiriki shughuli zote za kitaaluma na kijamii ambazo zitaanzishwa na serikali ya wanafunzi au uongozi wa Chuo. Shughuli hizo ni kama vile Michezo, bonanza, Tafrija mbalimbali, kutoa elimu ya afya kwa jamii na nyinginezo kadri zitakavyoanzishwa

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba na barua pepe zifuatazo:

Namba ya Chuo: 0743358048

Namba ya Mkuu wa Chuo: 0682487005

[*info@bphacoh.ac.tz*](mailto:info@bphacoh.ac.tz)

Nakutakia kila la kheri katika safari ya mafunzo katika Chuo cha afya Blue Pharma, karibu sana.

Imetolewa na:

BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH
PRINCIPAL
(BPHACOH)
P. O. Box 1570
SINGIDA

Gideon M. Samila

Mkuu wa Chuo

**KIAMBATANISHO NA 1: BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA CHUO CHA AFYA BLUE PHARMA**

Tarehe: ____/______/_______

Mkuu wa Chuo,
Blue Pharma College of Health,
S.L.P 1570,
Singida.

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA CHUO CHA AFYA BLUE PHARMA**

Mimi ______________________________________________________ (jina kamili) mwenye taarifa zifuatazo hapa chini:

Tarehe ya kuzaliwa: ____/_____/________Kutoka katika Mkoa wa: _________________________

Wilaya ya: _______________________ ambaye Mfadhili wangu ni ______________________________________________ (jina kamili) mwenye mawasiliano: _________________________________ (Namba ya simu inayopatikana).

Nimesoma maelekezo ya kwenye fomu ya kujiunga na Chuo cha afya Blue Pharma kilichopo Singida na kuelewa. Ninakubali kujiunga na Chuo cha afya Blue Pharma kwa ajili ya kusoma kozi ya stashahada ya Famasi na kuwa nitafuata Sheria na Kanuni za Chuo muda wote nitakapokuwa katika mafunzo.

Saini ya Mwanafunzi: _____________________________________________________________

Tarehe: ____________________________________________________________________________

**KIAMBATANISHONA 2: BARUA YA MFADHILI KUKIRI KUWA YEYE NDIYE ATAKUWA AKILIPA ADA NA MICHANGO MINGINE YA MWANAFUNZI**

Tarehe ______/______/______

Mkuu wa Chuo,
Blue Pharma College of Health,
S.L.P 1570,
Singida.

**YAH: KUKIRI KUFADHILI MASOMO YA MWANAFUNZI**

Mimi/ sisi

i. ____________________________________________________________________________

ii. ____________________________________________________________________________

iii. ____________________________________________________________________________

iv. ____________________________________________________________________________

Ninakiri/tunakiri kufadhili mafunzo ya Bw/Bi _____________________________________ (Jina kamili la mwanafunzi) ambaye amechaguliwa kujiunga Chuo cha afya Blue Pharma katika mwaka wa masomo 2025/2026 kwa ajili ya kusoma kozi ya stashahada ya Famasi. Pia Ninakiri/tunakiri kuwa nimesoma/tumesoma maelekezo ya fomu ya kujiunga na chuo pamoja na awamu za malipo ya ada na kuyaelewa.

| Na. | Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| i. | _________________________________ | __________________ | _______________ |
| ii. | _________________________________ | __________________ | _______________ |
| iii. | _________________________________ | __________________ | _______________ |
| iv. | _________________________________ | __________________ | _______________ |